



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO LA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI MEI, 2023

Mnatangaziwa kuwa mthani wa Usajili na leseni utafanyika siku ya tarehe **27/05/2023** katika vituo vilivyo anishwa kwenye jedwali hapo chini, Mthani huu ni kwa wahitimu waliomaliza mafunzo ya Uuguzi na Ukunga na kufaulu mitihani ya Wizara ya mwezi Machi, 2023 na wale wanaorudia.

Maombi ya mthani yatapokelewa rasmi kwa njia ya mtandao kwa kutumia o.tzmfumo wa Baraza <https://tnmcis.tnmc.go.tz> kuanzia tarehe **27/03/2023** hadi tarehe **10/05/2023**. Kila mtahiniwa atatakiwa kujaza fomu ya maombi (softcopy) na kulipia Shilingi 150,000/- kwa wanaoomba kufanya mthani huu kwa mara ya kwanza na Shilingi 75,000/- kwa wanaorudia. Watahiniwa wanaorudia wanashauriwa kuomba mthani kwa kutumia akaunti zao za awali.

Mnakumbushwa kuzingatia taratibu zote za maombi ambazo zimeainishwa kwenye mwongozo wa maombi ya mthani wa Usajili na Leseni ambao unapatikana kwenye tovuti ya Baraza www.tnmc.go.tz ikiwemo;

- Kuweka picha sahihi (passport size) yenye kivuli cha blue, **HD** ukubwa **35x35 mm** (Isiwe picha ya kupigwa kwa kutumia camera ya simu za mkononi)
- Kujaza majina sahihi kama yalivyo andikwa kwenye cheti chako cha **kidato cha nne**.

NB. Watahiniwa watakao kiuka vigezo na taratibu za kuomba mthani, maombi yao hayatapokelewa.

Nawatakia maandalizi mema.

Amama
Agnes Mtawa
MSAJILI
09/03/2023

JEDWALI LINALOONYESHA ORODHA YA VITUO VYA MITIHANI

SN	Kituo	Mkoa
1	Tandabui - Taasisi ya Afya Sayansi na Teknolojia	Mwanza
2	Chuo Kikuu cha Ualimu - DUCE	Dar es Salaam
3	Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji	Mbeya
4	Chuo Kikuu cha St. John	Dodoma